**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA WAZIRI MKUU – TAMISEMI**

**Namba za Simu**

**0784824983**

**0683934631**

**Shule ya Sekondari Mangaka**

**S.L.P 219**

**Tarehe……………..**

**Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi;**
**…………………………………………….................**
**S.L.P ……………………………………..**
**…………………………………………….**

Yah**: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI MANGAKA HALMASHAURI YA WILAYA YA NANYUMBU MKOA WA MTWARA MWAKA………….**

**1.** Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na kidato cha tano katika Shule hii mwaka…………. na atasoma tahasusi ya CBG/HKL/HGLi.

Shule ya Sekondari Mangaka ipo umbali wa Kilometa 01 Kaskazini mwa Mji wa Mangaka Usafiri wa basi kutoka mjini unapatikana katika kituo cha mabasi cha Mangaka, nauli ni Shilingi 2000/= kwa pikipiki au bajaji.
Muhula wa Masomo unaanza **tarehe................** hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni **tarehe.......................** Mwisho wa kuripoti ni **tarehe………………**

## 2. Mambo muhimu ya kuzingatia:-

### 2.1 SARE ZA SHULE

i. Sketi mbili za marinda box rangi ya kijani isiyoiva( kijani jeshi) -kitambaa kizito Cha suti; Sketi zinatakiwa kuwa ndefu zifike kwenye kiwiko Cha mguu.
ii. Mashati mawili meupe mikono mirefu.
iii. Hijab mbili rangi nyeupe kitambaa aina ya harua,ifunike kifua cha mwanafunzi pia iwe ndefu kufikia kifundo cha mkono akisimama.
iv. **SARE ZA MICHEZO;** ni T-shirt rangi ya dark blue isiyo na kola,Truck suit moja isiyobana mwili rangi ya dark blue pamoja na raba nyeupe jozi moja.
v. Viatu vya shule ni vyeusi vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi jozi mbili.
vi. Soksi jozi mbili nyeupe NDEFU zisizo na urembo au alama yoyote ya rangi;
vii. Tai mbili ndefu rangi ya kijani isiyoiva (zifanane na Sketi)
viii. Sweta Moja rangi ya kijani mikono mirefu isiyo na kola.
ix. **NGUO ZA KUSHINDIA(SHAMBA DRESS)**; Gauni mbili ndefu zenye mikono mifupi rangi ya damu ya mzee mshono wa solo: pamoja na hijab ya njano kwa wanafunzi waislamu.

x. T-shirt rangi ya kijivu aina ya "form six" yenye kola nyeusi inapatikana shuleni Kwa gharama ya Tsh. 20,000/=.

**NB. NI MARUFUKU KWA MWANAFUNZI KUJA NA NGUO ZA NYUMBANI SHULENI HATA ANAVOKUJA AVAE UNIFORM YA SHULE ALIYOSHONA (NGUO ZA KULALIA MFANO PAJAMA, SULUARI, SHIMIZI HAZIRUHUSIWI)**

### 2.2 Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja nayo shuleni:-

i. Madaftari 10 Counter books, kalamu na mkebe wa hesabu.
ii. **Ream (A4)** zinahitajika/zinatolewa mbili kwa mwaka (moja kwa kila muhura) zinapatikana shule kila ream Tsh.15,000/=
iii. Vitabu vya masomo ya tahasusi husika; hususani vitabu vilivyotolewa na Taasisi ya Elimu Tanzania**-** TIE (*orodha imeambatanishwa*);

iv. Dissecting Kit kwa wanafunzi wanaosoma Biology;
v. Scientific Calculator (FX 991) kwa wanafunzi wa sayansi.
vi. Godoro 1 la futi 2.5 kwa 6
vii. Mashuka Jozi 2: rangi ya light blue 1 na pink 1, blanket 1, foronya za godoro 2: ya blue 1 na pink 1, chandarua kimoja (1) rangi ya dackblue.
viii. Nguo za ndani za kutosha;
ix. Vyombo vya chakula (sahani, bakuli, kijiko na kikombe);
x. Ndoo 3 ndogo (lita Kumi) zenye mifuniko kwa ajili ya matumizi binafsi;
xi. Kwanja (Fyekeo) 1, jembe 1 lenye mpini, reki1 ngumu, mifagio 2 ya ndani (soft brooms) na 2 ya nje pamoja na brush ya chooni 1.
xii. Mafuta ya kupaka yasiyo na viambata vya sumu (cream)
xiii. Kanga au kitenge doti 1
xiv. Taulo,miswaki,dawa ya meno pamoja na sabuni ya kuogea na kufulia.
xv. Dawa yoyote ya chooni lita 5 kwa mwaka.
xvi. Nakala ya hati ya matokeo kidato Cha nne (Result Slip)
xvii. Nakala ya cheti Cha kuzaliwa
xviii. Picha 1 ya mwanafunzi, picha 4 za wazazi/walezi /ndugu wa karibu.
xix. Pasi ya mkaa
xx. Koti la maabara kwa wanafunzi wa CBG
xxi. Barakoa za kutosha kwa wanafunzi wa CBG kwa ajili ya kuvaa wakati wa mazoezi ya vitendo maabara
xxii. Gloves box moja Kwa ajili ya kujikinga wakati wa mazoezi ya vitendo wakiwa maabara.
xxiii. Bima ya Afya (kila mwanafunzi anatakiwa kuwa na bima ya afya, ambae hana anatakiwa kuja na Tsh 25000/= kwa ajili ya kukatiwa bima ya NHIF shuleni).

## 2.3 Michango mbalimbali

| **Na** | **Aina ya Mchango** | **Kiasi** |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | Tsh.65,000/= |
| 2. | Tahadhari | Tsh.8,000/= |
| 3. | Kitambulisho cha Shule | Tsh.7,000/= |
| 4 | **Jumla** | **Tsh.80,000/=** |

**Muhimu:** Michango yote ilipwe kwa njia ya benki ya **NMB** Jina la akaunti; **MANGAKA SEC.SCHOOL EDUCATION, Namba ya akaunti; 70501200073.** Usisahau kuandika jina kamili ya mwanafunzi anayelipiwa michango. Aidha utawasilisha risiti(Bank paying Slip) shuleni siku ya kuripoti.

## 3. Sheria na Kanuni muhimu za Shule

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya WAZIRI MKUU TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

### 3.1 Sheria na Kanuni za Shule

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.;
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;
iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku(Preparation);
iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;
v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
ix. Kutunza mali za shule;
x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na
xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

**MUHIMU:**

- ❖ **Mwanafunzi hapaswi kuja na SIMU shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;**

- ❖ **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;**

- ❖ **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa**).

**3.2 Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:**

i. Wizi;
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;
iv. Kutoa lugha chafu za matusi kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalim , mfanakazi wa taasisi au mtu yeyote yule;
vi. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni
vii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
viii. Uvutaji wa sigara;
ix. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa;
x. Kupata ujauzito au kutoa mimba;
xi. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
xii. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
xiii. Kumiliki, kukutwa au kutumia **simu** ya mkononi katika mazingira ya shule;
xiv. Kudharau Bendera ya Taifa;
xv. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na
xvi. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

4. **Viambata na Fomu Muhimu**
    i. Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali;
    ii. Fomu ya Maelezo Binafsi kuhusu Historia ya Mwanafunzi/Mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai;
    iii. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule; na
    iv. Picha nne (4) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na Namba zao za Simu.

5. Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

★ *Fomu hii inatakiwa irudishwe Kwa mkuu wa shule, pamoja na fomu zote zilizoambatanishwa zikiwa zimejazwa kwa usahihi.*

**Nakutakia maandalizi mema, karibu sana katika shule hii.**

**……………………………………….**

**MKUU WA SHULE**

NB: Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO: -

- Mkuu wa shule: 0784 824983
- Makamu Mkuu wa Shule : 0683934631
- Mwandamizi Taaluma: 0687 519 014
- Mwandamizi Malezi: 0755 487 578

**5.0 MEDICAL EXAMINATION FORM**

Mangaka Secondary School

P. O.BOX 219

**NANYUMBU- MASASI**

Date ................................

Ref. No.................................................

**PART A:**

To The Medical Officer;

..............................................................

............................................................

............................................................

REF: ...........................................................................................................................

Please examine to the above named student as to her physical and mental fitness for being student. Which by one way or another may affect a student for secondary school education.

1. a) eye sight b) hearing c) limbs d) speech e) Veneral disease f) leprosy and g) epilepsy

2. Neurosis3. Other serious diseases and 4. Pregnancy

**PART B: MEDICAL CERTIFICATE**

( To be completed by a government medical officer)

I have examined the above named student and consider that she is physically fit or not fit for full time secondary school education.

a) Eye sight ....................................................... f) Leprosy................................................

b) Hearing ...................................................... g) Epilepsy ...............................................

c) Limbs ............................................................ h) Neurosis.............................................

d) Speech......................................................... I) Other serious disease.........................

e) Veneral disease............................................. j) Pregnancy............................................

Date...................................................... Signature...........................................

Station ..................................................Designation ..........................................

Official stamp...............................................................

## 6.0 MAELEZO BINAFSI YA MWANAFUNZI

1.Jina kamili.........................................................................................................................(kama lilivyo kwenye self form)

2.Tarehe ya kuzaliwa .......................................................

3.Anwani ya nyumbani....................................................

4.Mahali unapoishi ( nyumbani) Mkoa.....................................Wilaya.......................................
Tarafa....................................Kata....................................Kijiji/mtaa.........................................

5. Shule ya sekondari unayotoka .........................................................................................

6.Dini/Dhehebu................................................................

7.Kabila...........................................................................

8.Utaifa: MTANZANIA/ SI MTANZANIA ( kata isiyohusika)

9.Jamaa katika familia:( Watakaoruhusiwa kumtembelea mwanafunzi awapo hapa shuleni)

1) Jina la Baba.........................................................................................................................

Anuani ......................................................... Namba ya simu .................................................

Mahali anapoishi................................................................ Kazi yake .......................................

2) Jina la mama ...........................................................

Anuani .................................................. Namba ya simu .......................................................

Mahali anapoishi.......................................Kazi yake .............................................................

3) Jina la mlezi/ndugu 1..........................................................................................................

Anuani ........................................................Namba ya simu........................................Mahali anapoishi.................................................................Kazi yake.....................................................

4. Jina la mlezi/ ndugu wa 2...................................................................................................

Anuani ........................................................Namba ya simu........................................Mahali anapoishi.................................................................Kazi yake.....................................................

**7 . MKATABA WA MWANAFUNZI KUTOSHIRIKI KATIKA MIGOMO, FUJO NA MAKOSA YA JINAI.**

Mimi..............................................................................................................................( Mwanafunzi) nakiri kuwa nimezisoma sheria , kanuni na taratibu za shule Kwa umakini na utulivu mkubwa.

Hivyo basi Ninaahidi nitazifuata sheria ,kanuni na taratibu za shule kama zilivyoelekezwa. Aidha naamini kuwa sheria na taratibu zipo Kwa nia ya kunisaidia katika nyanja zote muhimu ikiwa ni pamoja na nidhamu, maadili na taaluma. Vile vile naahidi kuwa sitoshiriki katika migomo, fujo,na makosa ya jinai kwa namna yoyote ile.Kinyume na hivyo hatua stahiki za kinidhamu zichukuliwe dhidi yangu.

Sahihi ya mwanafunzi............................................... Tarehe............................................

**8 . FOMU YA MZAZI/MLEZI KUKIRI KUKUBALIANA NA SHERIA, KANUNI NA MAELEKEZO YALIYOTOLEWA NA SHULE.**

Mimi.........................................................................................................................( Mzazi/mlezi) wa mwanafunzi.........................................................................................................................nakiri kuwa nakubaliana na sheria , kanuni na maelekezo yote yaliyotolewa na shule .

Hivyo basi niko tayari mtoto wangu asome katika shule hii, nitakuwa tayari kumpa kila aina ya msaada katika kufanikisha masomo yake na malezi yake kwa ujumla akiwa hapa shuleni kwa kipindi cha miaka miwili 02)

Sahihi ya mzazi............................................. .........Tarehe..........................................

**9. ORODHA YA VITABU**

| Na | SOMO | JINA LA KITABU |
|---|---|---|
| 1 | KISWAHILI | Kiswahili kidato cha tano (TIE-mtaala mpya 2024)<br>Kamusi ya kiswahili sanifu ya TUKI kubwa |
| 2 | GEOGRAPHY | Practical Geography Advanced Level(Map Reading,Photograph Interpretation,Field Research,Statistics and Introduction to Survey)**-T.I.E(new syllabus 2024)**<br>Physical Geography for Secondary Schools**-D.T Msabila**<br>Physical Geography for Secondary Schools**- T.I.E(new syllabus 2024)**<br>Practical geography**-ZISTI KAMILI** |
| 3 | ENGLISH LANGUAGE | Mgonja M.E(2025) competence in linguistic form five, mgonja lingua series. dar es salaam.<br>Dictionary (English to english)<br>English language (TIE) form five and form six |

| | | |
|---|---|---|
| 4 | BASIC APPLIED MATHEMATICS | Basic Applied Mathematics F5 and F6(T.I.E)**- T.I.E(new syllabus 2024)** |
| 5 | HISTORY | History for Secondary Schools Form Five(T.I.E new syllabus 2024) |
| 6 | HISTORIA YA TANZANIA NA MAADILI | historia ya tanzania na maadili (mtaala mpya 2024) |
| 7 | BIOLOGY | Biology for Advanced level(1999)4th Edition-Gl**assnand Suzan Tools,Nelson Thomas publisher,U.K**<br>BIOLOGICAL SCIENCE 3rd Edition Cambridge University Press<br>Understanding Biology |
| 8 | ACADEMIC COMMUNICATION | Academic communication form five na form six -TIE |
| | LITERATURE IN ENGLISH | literature in English (TIE) form five and form six |
| 9 | CHEMISTRY | CONCEPTUAL CHEMISTRY Volume I,Chand .S.(2014) New Delhi.S.Chand and Company PVT Ltd<br>Physical Chemistry -Advanced Level (TIE)<br>Organic Chemistry 1(Part A) T.I.E<br>In organic Chemistry T.I.E |

*NB.Mwanafunzi aje na Kitabu Kimoja au Zaidi Kwa Kila Somo kutokana na Tahasusi yake.*